

# **KCSE TRIAL 2020**

## **KISWAHILI PAPER 3**

### **SWALI LA KWANZA, SWALI LA LAZIMA**

#### **SEHEMU YA A: USHAIRI- (Alama 20)**

Niokoa muokozi, uniondolee mashaka

Kuyatukua siwezi, mjayo nimedhikika

Nimekitiri simanzi,ni katika kuudhika

Mja wako nasumbuka,nipate niyatakayo

Mja wako nasumbuka,nataka kwao afua

Nirehemu kwa haraka,nami nipate pumua

Naomba hisikitika,na mikono hiinua

Mtenda ndiwe moliwa,nipate niyatakayo

Mtenda ndiwe moliwa,we ndiwe mola wa anga

Mazito kuyaondoa,pamoja na kuyatenga

Ukauepusha ukiwa,ya pingu zilonifunya

Nikundulia muwanga,nipate niyatakayo

Nikundulia muwanga,nipate toka kizani

Na huzuni n'ondolea,itoke kwangu moyoni

Mambo mema niegheshea,maovu nisitamani

Nitendea wa manani,nipate niyatakayo

Igeuze yangunia,dhaifu unipe mema

Nili katika dunia,kwa afia na uzima

Moliwa nitimizia,yatimize yawe mema

Nifurahike mtima,nipate niyatakayo.

### **Maswali**

- (a). Eleza bahari zozote mbili za shairi hili (alama 4)
- (b). Eleza muundo wa shairi hili (Alama 4)
- (c). Mshairi ametumia uhuru wake wa utunzi. Eleza mifano minne huku ukitoa mifano (alama 4)
- (d). Andika ubeti wa pili katika lugha tutumbi (alama 4)
- (e). Fafanua dhamira ya mtunzi wa shairi hili (alama.2)
- (f). Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama ilivyotumika katika shairi (alama 2)
- (i). Nimedhihika
- (ii). Nifurahike mtima

### **SEHEMU B: RIWAYA – ASSUMPTAMATEI - CHOZI LA HERI**

2. Haki za watoto hazitiliwi maanane katika jamii nyingi za kiafrika. Eleza ukweli wa kauli hii kwa kurejelea Riwaya ya chozi la heri (Alama 20)

**au**

3. “Kuukata mkono niliostahili kuubusu yalinifika ya kunifika” (Alama 20)
- a. Eleza muktadha wa dondo hili (Alama 4)
- b. Eleza namna msemaji alivyoukata mkono aliostahili kuuibusu. (alama 6)
- (alama 14)
- c. Eleza tamathali ya usemi unaojitokeza katika dondo hili. (alama.2)
- d. Fafanua sifa nne za msemaji wa kauli hii (alama 8)

### **SEHEMU C: TATHILIA KIGOGO NA PAULINE KEA**

4. “Na hawa wafadhili wao nao lazima wavunje kambi zao. Sagamoyo twajeweza”

- a. Eleza muktadha wa dondo hili (alama 4)
- b. Kwa kutolea mifano saba kwenye tamthilia eleza jinsi kauli hii “Sagamoyo twajeweza” ni kinaya ? (alama 14)
- c. Mbali na kinaya tambua mbinu nyingine ya kisanaa katika dondo hili (alama 2)

**AU**

5. Jadili mbinu wanazotumia wanasagamoyo kujikomboa kutoka utawala dhalimu wa Majoka

(Alama 20)

**SEHEMU D: HADITHI FUPI - TUMBO LISILOSHIBA**

6. "... Ningeondoka.....mapema niende niibe au niue ili niwe mtu wa maana"

a) Eleza muktadha wa maneno haya (Alama 4)

b) Onyesha vile Kinaya kinavyojitokeza katika dondoo hili (Alama 2)

c) "Kinaya kimetumika kwingine katika hadithi husika. Thibitisha kwa kutumia hoja tisa

(Alama 9)

d). Eleza umuhimu wa msemaji katika hadithi hii (alama.5)

**AU**

7. (a). Eleza namna maudhui ya ndoa yalivysawiriwa katika hadithi ya Masharti ya Kisasa (alama 13)

(b). Kwa kurejelea hadithi ya Shibe inatumaliza,eleza namna maudhui ya ufisadi yanavyojitokeza

(alama 7)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

8 (a) Miviga ni nini? (Alama 2)

(b) Fafanua sifa sita za miviga (Alama 6)

(c) Kwa nini jamii huthamini miviga (Alama 8)

(d). Onyesha udhaifu unaohusishwa na miviga (Alama 4)

